Dunia Mpya

“Katika dunia mpya, ambamo haki hukaa, Mungu ataweka tayari makao ya milele waliokombolewa na mazingira makamilifu kwa maisha ya milele, upendo, furaha na kujifunza mbele zake. Kwa hapa Mungu mwenyewe atakaa pamoja na watu wake, na taabu na mauti vitakuwa vimepita. Pambano kuu litakuwa limemalizika, na dhambi haitakuwepo tena. Vitu vyote vyenye uhai na visivyo na uhai vitatangaza kwamba Mungu ni pendo, naye atatawala milele. Amina.” (2Pet. 3:13; Isa. 35, 65:17-25; Mt. 5:5; Ufu 21 :1-7, 22:1-5, 11:5).

Wengi wa wanadamu hudhani kwamba mbinguni ni bora kuliko kule kwingine. Hata hivyo kutokana na nuru ya Maandiko Matakatifu, nchi mpya ni ya kutamanika kuliko maisha tuliyonayo kwa sasa.

Maelezo ya Nchi Mpya

Nchi mpya ni kitu halisi
Sura mbili za kwanza za Biblia husimulia uumbaji wa Mungu wa maskani ya wanadamu iliyokuwa kamili. Sura mbili za mwisho za Biblia pia husimulia uumbaji mwingine mkamilifu wa maskani ya wanadamu, bali sasa utakuwa uumbaji mpya, baada ya ule wa awali kuharibiwa na dhambi. Mara zote, Biblia hutuambia kuwa maskani ya milele ya watakatifu ni mahali halisi, mahali ambako watu wakiwa na miili yao wataona, watasikia, watagusa, wataonja, watanusa, watapima, watapata picha, na kuifurahia. Waraka wa pili wa Petro sura ya tatu, unatoa muhtasari wa dunia tatu, ya kwanza ni ile kabla ya gharika, ya pili ni hii tuliyonayo itakayotakaswa kwa moto na ile ya tatu ni ile ambayo haki inatawala (2 Pet. 3: 6, 7, 13).

Kuendelea na kutofautiana. *Nchi mpya* huleta wazo kwamba dunia inaendelea kuwapo lakini inatofautiana na ile ya kwanza. Petro na Yohana waliona dunia ya awali ikitakaswa kwa moto, ikafanywa upya (2 Pet. 3:10 – 13, Uf. 21: 1). Ijapokuwa itafanywa mpya, itaendelea kujulikana – kwamba ni nyumbani. Pia itakuwa mpya kwa kuwa Mungu atakuwa ameondosha kila doa la dhambi.

Yerusalemu mpya. Yerusalemu mpya ni mji mkuu wa hii Nchi Mpya. Yerusalemu maana yake ni jiji la amani. Jina hilo limekosa maana kwenye dunia tuliyonayo leo. Katika nchi mpya, litaonyesha uhalisi wa amani.

Kiunganishi. Jiji hili litaunganisha mbingu mpya na nchi mpya. Kimsingi, mbingu humaanisha anga (Mwa. 1:20), anga la mbingu (Mwa.1:14-17), mbingu ya tatu ambako ndiko Paradiso (2 Kor. 12: 2-4). Mungu atajibu lile ombi kwenye sala ya BWANA, kwamba ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama mbinguni. Kwa kuiweka Yerusalemu Mpya kwenye Nchi Mpya, (Uf. 21: 1, 2) hatakuwa tu ameongezea nchi mpya umaridadi, bali pia atakuwa ameiinua Nchi Mpya ng’ambo ya ilivyokuwa, kabla ya kuanguka na kuifanya maskani Yake kutawala ulimwengu mzima. (Uf. 21:3)

Maelezo jinsi Yerusalemu mpya ilivyo
Yohana anasema Yerusalemu mpya itakuwa sawa na bibi arusi aliyepambwa kwa mumewe (Uf. 21: 2)

1. *Nuru yake.* Kitu cha kwanza alichoona Yohana ni nuru ya mji wa Yerusalemu. Mwana kondoo, mume wa bibi arusi aliyepambwa, ndiye nuru yake (Uf. 21:9, 11). Utukufu wa Mungu utaangazia mji kiasi cha kufanya mianga mingine kufifia (Uf. 21: 23, 24). Hakuna vichochoro vya giza (Uf. 21:25). Hapatahitajika, taa wala nuru ya jua, kwa Mungu mwenyewe atatoa nuru (Uf. 22:5)
2. *Ujenzi wake.* Mungu anatumia vito (madini) ya thamani nyingi kuujenga mji huu yaspi, kama bilauri (Uf. 21: 11, 18).Msingi wake umetegemezwa kwa vito aina 12, yaspi, yakuti samawi, kalkedoni, zumaridi, sardoniki, akiki, kriolitho, zabarajadi, yakuti ya manjano, krisopraso, hiakinto na amethisto. (Uf. 21: 19 -20). Hata hivyo, vito hivyo sivyo vyenye thamani kubwa. Mji umejengwa kwa dhahabu safi (Uf. 21: 18, 21). Malango 12 yataufanya mji kuingilika. Vipimo vya mji marefu, mapana na kwenda juu kwake ni sawasawa, kama maili 1,500. (Uf. 21: 15, 16)
3. *Vyakula vyake na maji yake.* Mto unatitirisha maji kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu, mto wa maji ya uzima (Uf. 22:1). Mti moja wa uzima kando ya kila upande wa mto, hutoa aina 12 tofauti za matunda ambazo zitawafanya wasizeeke wala kuchoka (Uf. 22:2, Mwa. 3:22). Walao matunda ya mti huu hawahitaji usiku kupumzika (Uf. 21:25), kwa kuwa katika nchi mpya hawatachoka.

Maskani yetu ya Milele

Biblia huweka wazi urithi wa watakatifu kuwa ni nchi. (Mt. 5;5, Zab. 37:9, 29, 115: 16). Yesu alikwenda kutuandalia mahali (Yoh. 14: 1 – 3), na kama tulivyoona, Maandiko Matakatifu huyaweka Maskani ya Mungu duniani (Uf. 21:2, 3, 5).

1. *Maskani ndani ya Jiji.* Jiji la Yerusalemu ndilo ambalo Ibrahimu alilitamani (Ebr. 11:10). Humo humo kuna makao mengi (Yoh. 14:2).

2. *Maskani kwenye nchi isiyo Jiji.* Watakatifu hawatazuiliwa ndani ya Jiji la Yerusalemu tu, kwa kuwa watairithi nchi. Kutoka ndani ya jiji watakwenda kubuni na kujenga nyumba zao (Isa. 65:21)

3. *Nyumbani pamoja na Mungu na Kristo.* Ahadi ya Yesu ya nilipo mimi nanyi mwepo itatimia (Yoh. 14:3). Makusudi ya Mungu kufanyika mwili (Yoh. 1: 14) yatatimia. Maskani ya Mungu na wanadamu, Mungu akiwa Mungu wao, na watu wakiwa watu wake (Uf. 21:3).

Maisha katika Nchi Mpya

1. *Kutawala pamoja na Mungu na Kristo* (Uf. 22:3-5, cf. 5:10)
2. *Shughuli za vitendo katika nchi mpya.* Tumekwisha kuona kuwa watakatifu watajenga (Isa. 65:21) ikiwa ni maana ya kubuni, kujenga, kuweka samani, kubadilisha muundo wa ujenzi na kadhalika. Mpango wa Mungu wa awali utarejeshwa. Huko mwanzo, Adamu alipewa kulima na kutunza bustani (Mwa. 2:15). Ukamilifu mtupu (Mw.1: 31)

Maisha ya Kijamii kwenye Nchi mpya

1. *Marafiki na familia.* Kutakuwa na kufahamiana. Ibrahimu, Isaka na Yakobo wataendelea kuwa na majina yao (Mt. 8:11). Bila shaka tutaendelea kusalimiana na wenzetu ambao kwa sasa tunashirikiana pamoja nao.

2. *Je, kutakuwako Ndoa?* Jibu la Yesu kwa swali la Masadukayo linasema hakutakuwa na ndoa kwenye nchi mpya. (Mt. 22:29, 30). Mungu hatanyima watu wake kilicho chema (Zab. 84:11). Kwa kuwa Mungu ni pendo, upendo wake utafurika nasi tutaufurahia (1 Yoh. 4:8,
Zab.
16:11)

Maisha ya Kiakili kwenye Nchi Mpya

1. *Je, kutakuwako Ndoa?* Majani ya mti yataponya mataifa (Uf. 22:2). Kuponywa kunakosemwa hapa ni kurejesha hali ya mwanadamu kurejea kutokana na kuharibiwa na dhambi. Hivyo uponyaji unamaana ya kuponya na akili pia kwa kuwa hapatakuwa na kuugua. (Isa. 33: 24, 20)

*2. Hapatakuwa na kikomo cha kuongeza maarifa. "*Mambo makuu ya ajabu yatafikiwa na hali ya juu ya mawazo na vifiko vyote vitafikiwa. Hata hivyo kutakuwa na mambo mengi ya ajabu ya kupekua. Kwa milele na milele kutakuwa na mafunzo yasiyo na mwisho wala hakuna kuchoka. Hazina zote za Mungu zitafunguliwa kwa wana wa Mungu waliokombolewa. Watatembea dunia nyingine bila kuwa na safari za kuchosha. Wana wa nchi hii wataingia katia ulimwengu wa wasiokuwa na dhambi na kushiriki maajabu ya elimu yao isiyokuwa na kasoro, ambayo wao wamekuwa nayo vizazi kwa vizazi". Ellen G. White Great Controversy *677*

3. *Maisha ya Kiroho kwenye Nchi Mpya.* Kama Yesu alivyokuja kutumika (Mt. 20:28), watakatifu watamtumikia Yesu (Ufu. 22:3). Sabato hata sabato watapata fursa ya kumwabudu Mungu. (Isa. 66:23).

Ambavyo Havitakuwako tena Kwenye Nchi Mpya

1. Maovu yote yataondoshwa Uf. 21: 4. Garantii kwamba dunia itabaki bila uovu ni kwa kuwa waovu hawataruhusiwa kuwemo (Uf. 21:8, Uf. 22:15). Alama itakayobaki ni makovu ya Yesu yanayotokana na kusulubiwa kwake. (Ellen G. White Great Controversy 677)

2. *Yaliyopita hayatakumbukwa (Isa. 65:17).* Uko ushahidi kwamba taabu ya maisha ya dunia hazitakumbukwa (Isa. 65:16). Mateso hayatainuka tena (Hab. 1: 9)

Thamani ya Imani katika Uumbaji Mpya

Imani katika uumbaji mpya huleta faida kwa mkristo: - **1.**Inampa ujasiri wa kuvumilia (Ebr. 12: 2, 2 Kor. 4: 16, 17). **2**.Huleta furaha na uhakika wa ijara (Mt. 5: 12, 1 Kor. 3: 14). **3**. Huimarisha kwa kutoa nguvu kuyapinga majaribu (Ebr. 11: 26). **4**. Inampa kuonja raha ya mbinguni kabla hajafika huko (2 Kor. 1:22, 2 Kor.5:5, Efe. 1: 14, Uf. 3:20). **5**. Huongoza kwenye utendaji wa juhudi. **6**. Hudhihirisha tabia ya Mungu. **7**. Hutuvuta kwa Mungu.

Daima Mpya

Ufalme utakuwa wa Mungu na Kristo wake. (Uf. 11:15). Hakuna yeyote atakayeruhusiwa kuupindua au kuwa mshirika kwenye utawala huo. (Dan. 2:44 Dan. 7:27). Kila kiumbe kitaungana kuimba na kumtukuza Mungu (Uf. 5: 13). "Mapambano makuu yamekoma. Dhambi na wenye dhambi hakuna tena. Ulimwengu mzima sasa umeshafika. Umoja na

ushirikiano ulio kamili kabisa umeenea ulimwenguni. Kutoka kwa Muumbaji hufurika uzima, nuru na furaha na kuenea mahali pote. Tangu kwa kitu kidogo mno mpaka kwa kikubwa kilinganacho na ulimwengu mzima, vitu vyote, vilivyo hai na visivyo hai, katika hali yote, hutangaza kuwa Mungu ni pendo.” (Ellen G. White Great Controversy 678).